

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Mtaa wa Mahakama,
S. L. P. 1419,
53103 MBEYA.
Simu: (025) 252503566
Nukushi: (025) 252502958
Barua pepe: rbcmbeya@pccb.go.tz
Wavuti: <http://www.pccb.go.tz>

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MBEYA – FEBRARI, 2021

WIZI WA DAWA ZA HOSPITALI WAMTIA HATIANI MUHUDUMU WA AFYA

Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Kyela imemtia hatiani muhudumu wa afya **Bi. Hilda Godfrey Nsasu** wa Hospitali ya Wilaya ya Kyela kwa makosa mawili.

Kosa la kwanza ni kosa la kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa wagonjwa waliokuwa wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kyela kosa ambalo ni kinyume na kifungu cha 15 cha sheria ya kuzuia na kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007, Kosa la pili ni wizi wa dawa na vifaa tiba vya Hospitali ya Wilaya ya Kyela kinyume na kifungu cha 258 na 270 vya Kanuni ya adhabu sura 16 (R.E 2019).

Mahakama imemtia hatiani **Bi. Hilda** katika makosa yote mawili na imemuhukumu kulipa faini ya shilingi 500,000/= kwa kila kosa au kwenda jela miaka mitatu kwa kila kosa. Bi. Hilda amelipa faini Tsh. 1,000,000/- na kuachiwa huru. Pamoja na maamuzi hayo Mahakama imetaifisha vifaa tiba pamoja na madawa.

Awali mtuhumiwa huyo alikamatwa na ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Kyela, tarehe 17/12/2020 kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ikiwa ni malalamiko kutoka kwa baadhi ya wagonjwa waliokuwa wamelazwa katika Hospitali ya wilaya Kyela kuwa amekuwa na tabia ya kuomba na kupokea rushwa.

Siku hiyo ya tarehe 17/12/2020 akiwa katika ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Kyela alionyesha hali ya wasiwasi iliyopelekea kumfanyia upekuzi kwenye begi lake alilokuwa nalo na kumkuta

na dawa mbalimbali, mali ya Hospitali ya Wilaya ya Kyela. Baada ya kumkuta na dawa hizo upekuzi zaidi ulifanyika nyumbani kwake kwa kuhusisha uongozi wa Hospitali ya Wilaya ambapo walifanikiwa kukuta dawa na vifaa tiba vya Hospitali ya Wilaya. Mhudumu huyo kwenye mahojiano na TAKUKURU alikiri kuiba dawa hizo.

Julieth Matechi

JULIETH MATECHI
MKUU WA TAKUKURU MKOA WA MBEYA
FEBRUARI 9, 2021
